# MISINGI YA UTUMISHI WENYE THAMANI NA MAADILI YA UTUMISHI WA UMMA TANZANIA

**NA JOHN STEPHEN**

# MALENGO YA MADA

Kuongeza uelewa wa Watumishi kuhusu Maadili, Uwajibikaji na Huduma Bora ili kuleta thamani katika Utumishi wa Umma

Kusisitiza umuhimu wa Maadili, Uwajibikaji na Huduma Bora kwa ustawi wa Taasisi na kuongeza thamani katika utumishi wa umma

Kutoa wito kwa Watumishi Kuzingatia Maadili, Uwajibikaji na Huduma Bora katika utoaji wa huduma kwa Umma ili kuleta thamani katika utumishi wa Umma Tanzania.

# UTUMISHI WA UMMA KATIKA DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO YA 2050

- Katika **Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050,** utumishi wa umma unalenga kujenga nguvu kazi ya kiwango cha juu inayojikita kwenye **weledi, uwajibikaji, ubunifu, na matumizi ya teknolojia** ili kusimamia uchumi shindani na jumuishi wenye lengo la kufikia hadhi ya nchi yenye kipato cha kati na hata cha juu

# UTUMISHI WENYE THAMANI NI NINI?

- Utumishi wenye thamani katika Utumishi wa Umma Tanzania ni dhana inayolenga kuhakikisha kuwa rasilimali za umma (fedha, muda, na nguvu kazi) zinatumika kwa ufanisi, tija, na uwajibikaji ili kutoa huduma bora na matokeo yaliyokusudiwa kwa wananchi

# MAANA YA THAMANI KATIKA UTUMISHI WA UMMA

- Katika utumishi wa umma Tanzania, **thamani** (values) zinamaanisha kanuni, maadili, au misingi inayoongoza tabia, maamuzi, na utendaji kazi wa watumishi wa umma.
- Thamani hizi huwekwa ili kuhakikisha utoaji wa huduma kwa umma unafanywa kwa weledi, uadilifu, na uwajibikaji.

- Kwa mujibu wa sharia, sera na miongozo ya utumishi wa umma Tanzania (kama vile Katiba, Sheria ya Utumishi wa Umma, na kanuni za Utumishi wa Umma), thamani kuu ni pamoja na:
- **Uadilifu (Integrity)** – Kutenda kwa uaminifu, kuwajibika, na kuepuka rushwa, upendeleo, au matumizi mabaya ya mamlaka.

- **Weledi (Professionalism)** – Kufanya kazi kwa ujuzi, usahihi, na kufuata taratibu za kitaalamu.
- **Usawa na Haki (Equity and Justice)** – Kuwahudumia wananchi wote bila ubaguzi wa kabila, dini, siasa, au hali ya kijamii.
- **Uwajibikaji (Accountability)** – Kuwajibika kwa matendo yako na matumizi ya rasilimali za umma.

- **Uwazi (Transparency)** – Kufanya maamuzi na shughuli za umma kwa njia wazi, inayoweza kuchunguzwa na umma.
- **Ufanisi na ubora** (Efficiency and Effectiveness) – Kutumia rasilimali kidogo kufikia malengo makubwa na kutoa huduma kwa wakati.
- **Huduma kwa Wateja (Customer Care)** – Kuwatendea wananchi kwa heshima, adabu, na kutatua malalamiko yao.

- Thamani hizi zinalenga kujenga utamaduni wa kazi unaoleta imani ya umma, kupunguza rushwa, na kuboresha maisha ya wananchi kupitia huduma bora za umma zinazotimizwa kwa kufundishwa kwa watumishi, kuwekwa kwa mwongozo wa maadili (code of ethics), na ukaguzi wa mara kwa mara.

# MAADILI NI NINI?

- Dhana ya maadili inazo tafsiri mbali mbali kulingana na mahitaji halisi ya jamii au kundi husika.
- Maadili ni **misingi au kanuni zilizokubaliwa katika jamii, taasisi au kundi fulani kama mwongozo wa mahusiano kati yao na namna wanavyofanya mambo yao.**

- Neno **Maadili** linahusu tabia au mwenendo. Kamusi ya Kiswahili Sanifu imetafsiri neno hilo kama ni **"Mwenendo mwema, mambo ya haki, usawa, mafundisho mazuri."** Mara nyingi maadili yanayotakiwa kuzingatiwa yametamkwa katika Sheria au Kanuni zilizowekwa maalum kwa ajili hiyo.
- Sheria na Kanuni hizi hutofautisha kati ya mwenendo unaofaa na ule usiofaa, na zimewekwa na kukubalika na Jamii, Serikali, Taasisi za Umma na zisizo za Umma ili zitumike kama vigezo vya tabia na mwenendo katika jamii.

- Kanuni hizi za maadili kwa kawaida hueleza ni mambo yapi yanakubalika na yapi hayakubaliki katika jamii husika kwa msingi wa uzuri au ubaya wake.
- Utumishi wa umma kama chombo chenye malengo yake na namna ya kuyafikia, kimejiwekea kanuni za msingi ambazo zitawezesha kufikia malengo yake. Hizo ndizo zinaunda **MAADILI YA UTUMISHI WA UMMA.**

- Ukiukwaji wa kanuni za maadli kwa watumishi ni kosa na aina ya adhabu inayoweza kutolewa inategemea na uzito wa kosa lililofanyika ambapo baadhi ya makosa yanaweza kushughulikiwa na mamlaka za kawaida kwa kuchukua hatua za kiutawala na kinidhamu (mf kuchelewa kazini, kutoonekana kazini, n.k.)

- Makosa mengine makubwa kama **wizi, kupokea rushwa au kupigana** yanaweza kupelekea mtumishi kushtakiwa kwenye mamlaka za dola au hata kufungwa. **Kanuni ya 65** kwenye **kanuni za utumishi wa umma** na **sera ya menejimenti na ajira (1999)** kwa pamoja vimesisitiza wajibu wa watumishi wa umma kuwa waadilifu ili kujiepusha na matatizo yanayoweza kuwapata kwa kukosa uadilifu

- Maadili ni misingi, kanuni na taratibu zilizokubalika katika jamii au kundi fulani kama mwongozo wa mahusiano kati yao na namna wanavyofanya mambo yao.
- Kanuni hizo ni kama vile uaminifu, uadilifu, ukweli, uwajibikaji, staha, heshima, n.k.
- Utu!
- Maadili ni viwango vya utendaji vinavyokuongoza katika kufanya kilicho sahihi na kuwa na tabia au mwenendo mwema.

# CHIMBUKO LA MAADILI NA UWAJIBIKAJI KATIKA UTUMISHI WA UMMA WENYE THAMANI NCHINI TANZANIA

- Maadili ya Utumishi wa Umma na Uwajibikaji ni mambo ya Kisera na Sheria
- **Sera ya Menejimenti na Ajira ya mwaka 1999;**
- Marekebisho ya sheria ya **UU. No.8/2002 kupita rekebisho Namba 18/2007 na Usimikwaji wa OPRAS/PEPMIS**

- **Kanuni ya 65** ya **Kanuni za Utumishi wa Umma 2022** (Jedwali la Tatu)
- Msisitizo ni juu ya “Kufanya Kilicho Sahihi” kwa;
  - Kuzingatia utaalam,
  - Kuwa waaminifu na
  - Kuwajibika

# THAMANI NA MAADILI YA UTUMISHI WA UMMA

Katika utumishi wa umma, kuna kanuni nane (8) za Maadili:-

1. Kutoa Huduma Bora
2. Utii kwa serikali
3. Bidii ya kazi
4. Kutoa huduma bila upendeleo
5. Kufanya kazi kwa uadilifu
6. Kuwajibika kwa umma
7. Kuheshimu sheria
8. Matumizi sahihi ya taarifa

# MISINGI YA MAADILI YA UTUMISHI WA UMMA

**Kuzingatia Utaalam ( Professionalism)**

**Uaminifu (Honesty)**

**Kutimiza Wajibu (Responsibility)**

# MISINGI YA MAADILI ...

**Kuzingatia Utaalam**

- Kutoa huduma bora
- Bidii ya kazi
- Kutoa huduma bila upendeleo
- Matumizi Sahihi ya Taarifa

## Uaminifu

- Kufanya kazi kwa uadilifu

## Uwajibikaji

- Utii kwa Serikali
- Kuwajibika kwa umma
- Kuheshimu sheria

# Msingi wa Kwanza: Kuzingatia Utaalam (PROFESSIONALISM)

## Kanuni ya 1: Kutoa Huduma Bora

Vigezo vya Huduma Bora

- Huduma kupatikana
- Muda kuzingatiwa
- Kuzingatia Viwango
- Kutoa huduma kwa heshima
- Lugha:Mavazi

# Kutoa Huduma Bora: Muda kuzingatiwa

Epuka Matumizi mabaya ya Muda wa Kazi

Huduma kwa wakati na kufikia matarajio ya wateja





# Kutoa Huduma Bora….

Kujali Wateja kwa:

- Kukaribisha kwa furaha na upendo
- Kusikiliza na kuelewa tatizo lake
- Kutoa maelekezo kwa Lugha nzuri
- Kuvaa mavazi ya heshima

# Kutoa Huduma Bora:Mavazi ya Heshima





# Heshima … (Mavazi)





JAMHURI YA MUUNGANO
WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA.

# MWONGOZO WA MAVAZI KWA WATUMISHI WA UMMA KWA MUJIBU WA WARAKA WA UTUMISHI WA UMMA Na. 3 MWAKA 2007.

## BAADHI YA MAVAZI YASIYOFAA KWA WANAUME




## BAADHI YA MAVAZI YASIYOFAA KWA WANAUME

- Nguo ambazo ni za kazi maalum kama vile michezo (Hizi zivaliwe wakati wa shughuli hiyo tu.)
- Nguo ambazo zina michoro, maandishi na picha ambazo haziendani na shughuli za serikali.
- Nguo zinazobana.
- Kaptura ya aina yoyote.
- Suruali yoyote inayoachwa bila kupindwa.
- Suruali za "Jeans" na Fulana "T-shirts" (Hizi zivaliwe tu wakati wa shughuli maalum inayotambulika)
- Kikoi au msuli.
- Nguo zenye maandishi ya chama chochote cha siasa na yenye kuonyesha ushabiki wa kitu fulani.
- Nguo yoyote inayopingana na maadili ya utumishi wa umma.

JAMHURI YA MUUNGANO
WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA.

MWONGOZO WA MAVAZI KWA WATUMISHI WA UMMA KWA MUJIBU WA WARAKA WA UTUMISHI WA UMMA Na. 3 MWAKA 2007.

## BAADHI YA MAVAZI YASIYOFAA KWA WANAWAKE



## BAADHI YA MAVAZI YASIYOFAA KWA WANAWAKE

- Nguo zinazobana.
- Nguo fupi ambazo zinaacha magoti wazi.
- Nguo ambazo zinaacha sehemu ya mwili wazi kama vile kitovu na kifua.
- Nguo ambazo zina picha, michoro, na maandishi ambayo hayaendani na shughuli za serikali.
- Kaptura aina yoyote ile kama vile pedo na pensi.
- Nguo zinazoonyesha maungo ya mwili (transparent).
- Suruali za 'Jeans'
- Suruali yoyote iliyoachwa bila kupindwa.
- Fulana – 'T-Shirts' (Hizi zivaliwe tu wakati wa shughuli maalumu inayotambulika.)

# Kutoa Huduma bora …

- ❑ Ushirikiano ili kuwa na utendaji wa pamoja (Team Work)
  - ➢ Ni muhimu kuwa na Vikao vya mara kwa mara kujadili utendaji kazi ili kubaini mafanikio na changamoto
  - ➢ Kuheshimu nafasi ya kila mmoja katika kufanikisha utoaji wa Huduma

# Kutoa Huduma Bora ……

- Malengo halisi ya kazi yanayopimika(PEPMIS/Mkataba wa Utendaji Kazi Serikalini);
- Uelewa wa kazi yako (competence);
- Uelewa wa pamoja kuhusu Dira na Dhamira ya Taasisi na mikakati ya utekelezaji. ***WATUMISHI WOTE MNATAKIWA KUFAHAMU DIRA, DHIMA NA MAADILI YA TAASISI UNAYOFANYIA KAZI. (Mf. Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali OSG)***

# Huduma Bora: Utendaji wa Pamoja



# Kanuni ya 2: Kufanya Kazi kwa Bidii

- Matumizi sahihi ya muda wa kazi:Shughuli binafsi zifanywe baada ya saa za kazi
- Kujali muda wa kazi na kufika kazini mapema
- Kuondoka baada ya kukamilisha kazi.
- Kutulia ofisini na kufanya kazi
- Kumhudumia Mteja ipasavyo

# Bidii ya Kazi:Matumizi ya Muda wa Ofisi



# Bidii ya Kazi…

- Kuwa tayari kufanya kazi kwenye kituo chochote cha kazi utakachopangiwa. (***Ref. Reg. 107 of PSR, 2022 and SO,2009)***
- Kufanya kazi kwa **ufanisi** ikiwemo kukamilisha majukumu kwa wakati
- Kutumia Utaalamu, Ujuzi na Maarifa kuongeza tija kazini

# Kutoa Huduma bila Upendeleo

- **Haki ya kuwa mwanachama** wa Chama cha Siasa
- **Haki ina mipaka**: Mfano – Taarifa za kikazi zisipelekwe kwenye Vyama vya Siasa
- **Haki ya kuamini** dini yoyote inayokubalika
- **Kuepuka upendeleo** wa aina yoyote sehemu za Kazi:udini, ukanda, ukabila,Itikadi ya Kisiasa, Jinsi, n.k

***Kwa wanaotaka kugombea nafasi za uongozi wa Kisiasa*** wanapaswa kuzingatia **Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na. 1 wa Mwaka 2015.**

- **Ubunge wa Majimbo / Ubunge wa Viti Maalumu** – Kuacha Kazi baada ya kutangazwa na Tume ya Uchaguzi kuwa Mgombea.
- **Afrika Mashariki – Kuacha Kazi na kulipwa Mafao yake kuanzia siku atakayoteuliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki.**

- **Udiwani** - Kuacha Kazi baada ya kutangazwa na Tume ya Uchaguzi kuwa Mgombea.
- **Ubunge wa kuteuliwa na Rais** – ana hiari ya kuchukua likizo bila malipo kwa kipindi chote cha ubunge au kuacha kazi na kulipwa mafao kuanzia siku atakayoteuliwa kuwa Mbunge.
- **Udiwani wa kuteuliwa na Waziri mwenye dhamana ya TAMISEMI** - ana hiari ya kuchukua likizo bila malipo kwa kipindi chote cha kuwa diwani au kuacha kazi na kulipwa mafao kuanzia siku atakayoteuliwa kuwa Diwani.

# Kutoa Huduma bila Upendeleo

- Nafasi yoyote ya Uongozi katika Chama cha Siasa- kuacha kazi na kulipwa mafao

# Matumizi sahihi ya taarifa

Utunzaji siri za Ofisi (Sheria ya Usalama wa Taifa Namba 3/1970 Kifungu cha 5 (a) na (b): Kifungo kisichozidi miaka miaka 20!

- Kutoa Taarifa kwa wahusika/wadau pale ambapo zinawahusu
- Kuepuka kutumia taarifa kwa manufaa binafsi (kuuza, umaarufu)

- **Changamoto:** Kushindwa kutunza siri kutokana na uzembe na kukosa umakini wakati wa kutumia TEKNOHAMA.
- Watumishi wa Umma wanapaswa kuzingatia MWONGOZO WA MATUMIZI BORA, SAHIHI NA SALAMA WA VIFAA, DATA NA MIFUMO YA TEHAMA SERIKALINI 2022 ambapo:-

- Anuani za barua pepe anuani binafsi km yahoo.com,gmail.com,n.k haziruhusiwi kutumika katika mawasiliano ya Serikali. Tumia barua pepe za Kiserikali tu.
- Barua na nyaraka zote za Siri (Confidential) zisitumwe kwa njia ya barua pepe.
- Internet cafe zisitumike kutuma taarifa za Serikali n.k

# UAMINIFU (HONESTY)

- Matumizi ya Madaraka na Ofisi kwa manufaa ya umma na siyo binafsi
- Matumizi ya Fedha na Raslimali nyingine za umma kwa manufaa ya Umma na siyo binafsi.

# Kufanya kazi kwa Uadilifu….

- Vitendo vya kuivunjia heshima Serikali - mfano:
- Ulevi,



# Kufanya Kazi kwa Uadilifu: kuepuka Ulevi….



Pia kuepuka mambo yafuatayo:

- Kupigana hadharani, uchafu wa mwili na nguo
- Kukopa hadi kushindwa kulipa.
- Kuomba au kupokea Rushwa
- Zawadi

# Kwa nini si sahihi kupokea zawadi?

(i) Huduma inayotolewa tayari imelipiwa ujira halali;

(ii) Inasababisha kutokuzingatia haki kwa watu wengine;

(iii) Kujenga mazoea na hatimaye kuhalalisha upokeaji wa zawadi na kuwa rushwa;

(iv) Kuharibu uadilifu na heshima yako kama mtumishi; na

(v) Kushindwa kuheshimu sheria, kanuni na taratibu

# Msingi wa Tatu: Kutimiza Wajibu (RESPONSIBILITY)

## Utii kwa Serikali…

- Kutii Serikali iliyopo madarakani kwa kuheshimu na kutekeleza Sera na maelekezo ya viongozi wa Serikali;
- Kupokea na kutekeleza maagizo yaliyo halali (lawful instructions); na
- Kushauri kwa maandishi juu ya maagizo ambayo si halali au yasiyo na maslahi kwa Umma.

# Kuwajibika kwa Umma

- Kujihesabu kuwa watumishi wa umma



IMEANDALIWA NA JOHN STEPHEN

# Mwonekano wa mteja siyo kigezo!!





# Kuwajibika kwa Umma

- Kuwahudumia wateja na watumishi wenzio kwa heshima
- Umakini kwa wananchi wenye mahitaji maalumu (Wazee, Wajawazito, Walemavu n.k)
- Kuacha dharau,ubabaishaji na unyanyasaji kwa wananchi wakati wa kutoa huduma

# Kuheshimu Sheria

- Ufahamu wa sheria:Sheria za Sekta na Sheria za Utumishi wa Umma n.k
- Kutoa taarifa kwa mamlaka kuhusu maagizo ya kuvunja sheria, kanuni au taratibu, na
- Kuzingatia kikamilifu sheria zinazotawala Utumishi wetu

## Kuheshimu Sheria…

- **Mapenzi Kazini**

Kujiepusha kabisa na mahusiano ya kimapenzi sehemu za kazi

*Mahusiano ya Kimapenzi?*

“ *Hivi kama nina uhusiano wa kimapenzi na mtumishi mwenzangu sehemu za kazi lakini kazi tunachapa kama kawaida, kuna ubaya wowote?*

# Kuheshimu Sheria…

## **Mapenzi mahali pa kazi!**





# Unyanyasaji hauchagui jinsi



# Kuheshimu Sheria…

Kwa nini si sahihi kuwa uhusiano wa kimapenzi kazini?

- Kuharibika kwa mahusiano kazini,
- Kuathirika kwa utendaji,
- Upendeleo na matumizi mabaya ya rasilimali.
- Kuharibu sifa na kuiletea aibu Taasisi na Serikali, na
- **Hatari ya maambukizi ya ukimwi na kuathiri nguvu kazi kutokana ugonjwa na vifo.**

# Hali ya Kimaadili Tanzania

- Maoni ya Watumishi katika Mikoa 12 na Halmashauri zake kati ya 2009 – 2012:-

1. Ucheleweshaji wa Huduma;
2. Tabia zinazowaudhi wateja- dharau, maringo, lugha chafu;
3. Upendeleo kwa misingi ya ukabila, udini;
4. Rushwa; na
5. Kukosekana kwa vikao kwa ajili ya kutoa mrejesho.

# Hali ya Kimaadili….

- Ufuatiliaji wa maoni ya wananchi 2014 chini ya OR-MUU ulionesha:-

1. Matumizi mabaya ya Madaraka;
2. Rushwa (Jamii kutukuza Maovu);
3. Matumizi mabaya ya rasilimali za umma;
4. Wasimamizi/Mamlaka kutochukua hatua za Nidhamu kwa wakati

*Kiwango cha uzingatiaji wa Maadili kufikia 66.1% (+9.2%).*

# 4.0 CHANGAMOTO NA HATUA ZA KUCHUKUA

*4.1 Changamoto*

i. Wananchi kutofahamu haki na wajibu wao -Huduma kutafsiriwa vibaya;
ii. Kutoripoti vitendo vya ukiukwaji wa Maadili ikiwemo vitendo vya rushwa;
iii. Baadhi ya wasimamizi kutowachukulia hatua wanaokiuka Maadili;
iv. Ufinyu wa bajeti au kutotumia vizuri fedha zinazopatikana.
v. Tabia binafsi na malezi mabaya kuanzia ngazi ya familia ***' Samaki Mkunje angali mbichi'***

# Changamoto na Hatua…

*4.2 Hatua za kuchukua*

(a) Wajibu wa Menejimenti- usimamizi na mifumo thabiti:-

- Mafunzo ya Maadili kwa watumishi, hasa mtumishi anapoanza kazi.
- Uteuzi wa Maafisa wa Maadili – Waraka wa Utumishi Na.1 wa Mwaka 2015 na Mwongozo wa Ufuatiliaji wa Uzingatiaji wa Maadili katika Utumishi wa Umma 2014;

- Kuimarisha mifumo ya uwajibikaji, Kamati za Uadilifu;
- Kuanzisha au Kuimarisha Dawati/Ofisi ya Malalamiko – Mwongozo wa Ushughulikiaji wa Malalamiko ya Wananchi katika Utumishi wa Umma; na
- Tuzo na Hatua za Kinidhamu kulingana na Kanuni za Utumishi wa Umma 2003;

# Changamoto na Hatua …

(b) Wajibu wa kila mtumishi- kuzingatia taratibu, kutoa taarifa.

(c)Wajibu wa Jamii – malezi sahihi, kukemea maovu na kushirikiana na Serikali kufichua uovu.

## HITIMISHO

# KISA KUHUSU MAADILI

## Ndugu MAJIVUNO MUHENGA

Ni Afisa Mwandamizi katika Cheo chake ni Afisa Ugavi Mkuu, Amefanya kazi kwa zaidi ya miaka 30 kwa uadilifu wa hali ya Juu, akiwa amebakiza miezi tisa kustaafu, anawaza kwamba hajajiandaa vema kustaafu, anaamua "liwalo na liwe" mbona wengine wanapokea?

Ananaswa na Mtego wa Rushwa ya Shs. 500,000/= aliyopewa kwa ajili ya "kutoa zabuni kwa Upendeleo"

**Anakamatwa na TAKUKURU, kushtakiwa na kuhukumiwa kifungo cha miaka 3 Jela. Anapoteza haki zake zote masikini ikiwamo PENSHENI yake! ( Kanuni ya 40(2) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022)**

**Je, Uadilifu Bw. MAJIVUNO wa miaka 30 una faida yoyote? Na tunapata funzo gani??**

# JITATHMINI NA KUCHUKUA HATUA

***USIPOTEZE MUDA, BADILIKA SASA NA KUWA MTUMISHI MWADILIFU ILI UTUMISHI WA UMMA UONEKANE WA THAMANI SIKU ZOTE.***

# AHSANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA

